# Sera ya Uzuizi wa Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia (PSEA)

**Nambari ya Sera:** 405
**Tarehe rasmi ya Kuanza:** Julai 2020
**Tarehe Itakayofuata ya Mapitio ya Pili:** Julai 2022
**Mmiliki wa Sera:** Afisa Mkuu wa Maadili na Matekelezo

*Sera hii inatangulia sera zote za awali zinazohusiana na kuzuia na kushughulikia dhuluma na unyanyasaji wa kijinsia. Sera hii pamoja na Sera za Kulinda Mtoto na Kupampana na Ubaguzi na Kupampana na Mateso, ambazo zina shughulikia tabia zingine zililozopigwa marufuku.*

## Lengo

Pact imejitolea kuzia aina zote za dhuluma na unyanyasaji wa kijinsia (SEA). Sera hii inatafuta kuhakikisha kwamba washirika wote wa miradi ya Pact wako salama na hawata wekwa hatarini au kwa mwenendo unao husiana na dhuluma au unyanyasaji wa kijinsia. Tumejitolea kushughulikia kwa upesi na kwa makini madai yeyote ya dhuluma na unyanyasaji wa kijinsia.

## Matumizi

Sera hii inatumika kwa wafanyikazi, washauri, wakandarasi huru, wakala na wanaojitolea wote kwa kijumla ("Wafanyikazi"), na wageni ("Wageni") ambao hufanya kazi kwa au kutembelea Pact na miradi ya wakandarasi wadogo wa Pact.

## Mahitaji

### *Ufafanuzi*

Unyanyasaji wa kijinsia ina fasiliwa kama dhuluma halisi au ya kujaribiwa kutoka kwa nafasi ya mamlaka au uaminifu, kwa lengo la ngono. Unyanyasaji inaweza jumuisha kufaidika kifedha, kijamii, au kisiasa kutoka kwa dhuluma ya kijinsia kwa mwingine. Dhuluma ya kijinsia ina fasiliwa kama uingiliaji halisi au wa kudhaniwa wa hali ya ngono, aidha kwa mabavu au chini ya hali isio sawa au ya kulazimishwa.

### *Mifano ya Tabia Zilizopigwa Marufuku*

Wafanyikazi na Wageni wa Pact wamepigwa marufuku kushiriki na aina yeyote ya dhuluma au unyanyasaji wa kijinsia kwa mtu anayejihusisha na Pact au na mradi wa mkandarasi mdogo wa Pact. Usijijihusishe na uhusiano wa kijinsia na wanaofaidika na mradi, kwa vile uhusiano hizi zinategemea hali za uwezo usio sawa kwa undani.

Mifano ya dhuluma na unyanyasaji wa kijinsia inajumuisha, lakini sio hizi pekee:

- Dhuluma au unyanyasaji wa kijinsia;
- Mguso wa aina ya kijinsia usiotakikana (bila idhini);
- Kudai ngono katika muktadha wowote;
- Kufanya ngono kuwa kigezo cha msaada au kushiriki katika mradi wa maendeleo;
- Kulazimisha mtu kufanya ngono;
- Kulazimisha mtu kushiriki katika kazi ya ngono au ponografia.

### *Kuripoti ya Lazima*

Wafanyikazi na Wageni wanahitajika kuripoti tuhuma au madai ya Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia, au kutofuata sheria na sera hii, ndani ya saa 24 kwa kuarifu Afisa Mkuu wa Maadili na

Matekelezo au kwa kutuma ripoti kwa [Mfumo wa Sehemu ya Kuripoti Maadili](). Wafanyikazi na Wageni pia wanapaswa kuripoti madai ya kale ya Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia kutoka kwa mradi wowote wa Pact.

Ripoti zote za Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia zinajumuisha zifuatazo:

- Je, ni nani alitenda makosa yanayodaiwa?
- Je, unajua kama kuna mtu mwingine anayehusika?
- Ni nini kilicho tendeka? Elezea kwa makini kile unacho fahamu au kushuku kuhusu tukio la Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia.
- Je, kulikuwa na mashahidi wowote?
- Je, ni wakati gani na ni wapi tukio hilo lilitendeka? Peana tarehe na wakati, kama inawezekana.

## Majukumu ya Wafanyikazi

Wafanyikazi ni lazima:

- Wawe makini kuhusu visa vinavyo shukiwa vya Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia ndani ya idadi ya watu iliyo hatarini.
- Kuripoti matukio yeyote ya kushukiwa au uwezekano wa dalili za Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia.
- Kamwe usisite kuripoti kushukiwa kwa Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia kwa sababu ushahidi huku kusanywa.
- Heshimu utu, mapenzi na haki za manusura wa Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia, ikiwemo mapenzi yao kuhusu kuripoti kwa watu wengine.
- Tafuta ushauri kutoka kwa Ofisi ya Pact ya Maadili & Matekelezo na maswali kuhusu kama au vipi kuripoti visa vinavyo shukiwa.

### *Muundo wa Mradi*

Wafanyikazi wa Pact wenye majukumu ya kuunda, kupanga bei, kugharamia, na kutekeleza miradi, moja kwa moja au sio moja kwa moja kupitia wakandarasi wadogo, wana majukumu ya kuhakikisha kwamba wakala, washirika, na wakandarasi wadogo wetu wako na sera za PSEA.

### *Ofisi za Nchi*

Afisi zote za Pact zinahitajika kutambua rasilimali za usaidizi za dharura au za manusura katika nchi yao, kama inawezekana, kutumia kama kuna tukio la madai ya Dhaluma na Unyanyasaji wa Kijinsia, na manusura katika kesi hii anataka kujitambulisha kwa rasilimali hizo. Mkurugenzi wa Nchi (CD) ana majukumu ya kutambua rasilimali za usaidizi za dharura na za manusura katika nchi yao, kama inawezekana, kushughulikia na kuripoti ukiukaji unao shukiwa kuhusu Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia, na kufanya wafanyikazi watambue rasilimali hizi.

### *Uchunguzi na Ufuatiliaji*

Ofisi ya Maadili & Matekelezo ina wajibu wa kuhakikisha kwamba madai ya Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia yana chunguzwa kulingana na sera hii. Katika uchunguzi wote, Wafanyikazi na Wageni wanahitajika kushirikiana katika uchunguzi. Hadi pale itakapo hitajika na Ofisi ya Maadili & Matekelezo au utekelezaji wa sheria, habari zote zinapaswa kuhifadhiwa kwa usiri kuhusu mnusura (manusura) shukiwa na mhalifu (wahalifu) shukiwa.

Afisa Mkuu wa Pact wa Maadili na Matekelezo na wachunguzi wao wana majukumu ya kutekeleza uchunguzi wa ripoti za ndani za Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia hadi pale mamlaka ya maeneo hayo hawahusiki. Afisa Mkuu wa Maadili na Matekelezo ni lazima aripoti

muhtasari wa data ya matukio kwa Timu ya Wasimamizi Wakuu wa Pact (SMT) na kwa Baraza la Wakurugenzi kila baada ya miezi minne. Afisa Mkuu wa Maadili na Matekelezo aripoti mara moja kesi zote za kipekee kwa SMT na kwa Baraza la Wakurugenzi kama itakavyo hitajika.

Afisa wa Maadili na Matekelezo pia ana wajibu wa kufuatilia ya kwamba sera hii inazingatiwa mara kwa mara.

### Utekelezaji

Dhuluma na/au unyanyasaji wa kijinsia wa washirika wa mradi inachangia vitendo vya makosa makubwa na ni chanzo cha kupewa nidhamu, ikiwemo kufutwa ajira na kupelekwa kwa watekelezaji sheria, na pia kusitisha kwa misaada ya wakandarasi wadogo, kama itakuwepo. Afisi za Nchi ni lazima zizingatie sheria za maeneo kuhusu ukiukaji wa Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia.

Mfanyikazi aliye dhibitishwa kwamba amenyanyasa na/au amedhulumu kijinsia atafutwa ajira katika Pact na hataweza tena kupewa ajira. Kama madai yamefanywa kwa nia mbaya, hatua zifaazo zitachukuliwa kufuatilia mtu aliyefanya madai hayo na mtu aliyeshtakiwa. Mfanyikazi yeyote anaye peana mashataka kwa nia mbaya au ya uwongo atapewa nidhamu, hadi kufutwa ajira.

### Rasilimali Zinazohusika

- Pact imejitolea kudumisha Kijitabu cha Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Hatua maalum za ulinzi dhidi ya dhuluma za kijinsia na unyanyasaji wa kijinsia (ST/SGB/2003/13) na the Kamati ya Uwakala Wakusimama Wakushirikiana (IASC) Kanuni Sita Kuu Zinazohusiana na Dhuluma na Unyanyasji wa Kijinsia, 2019.